GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE


JUZU NO. 238 **Sha'ban-Ramdan** 1445 **AH** **Machi–** 2024 **Amman** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

Nimekuja kupanda mbegu tu, basi ile mbegu imepandwa kwa mkono wangu, hivyo utakua na kustawi na hakuna awezaye kuuzuia



Nimekuja kupanda tu mbegu,basi ule mbegu umepandwa kwa mkono wangu hivyo itakua na kustawi na hakuna awezaye kuizuia

Enyi nyote, kumbukeni kwamba hii ni bishara ya yule aliyeumba ardhi na mbingu, kwamba ataeneza jumuiya yake hii katika nchi zote, na kuwapa ushindi juu ya wote kwa dalili na ushahidi. Siku zinakaribia ambapo hili litakuwa dhehebu pekee ulimwenguni ambalo litakumbukwa kwa heshima. Mwenyezi Mungu atalibariki dhehebu hili na Silsila hii kwa namna ya hali ya juu na isiyo ya kawaida na kila anayetaka maangamizo yake, atamfedhehesha. Na ushindi hii utadumu milele hadi siku ya Kiyama itokee. Kumbukeni kuwa hakuna atakayeshuka kutoka mbinguni. Wapinzani wetu wote waliohai leo, wote watakufa na hakuna hata mmoja wao atakayemwona Yesu mwana wa Mariamu akishuka kutoka mbinguni kisha kizazi chao kitakachobakia pia kitakufa na hakuna hata mmoja wao atakayemuona Isa bin Maryam akishuka kutoka mbinguni. Na kisha watoto wa watoto wao watakufa. Nao pia hawatamwona mwana wa Mariamu akishuka kutoka mbinguni. Ndipo Mungu atatia hofu mioyoni mwao kwamba wakati wa kutawaliwa kwa msalaba pia umepita. Na dunia ikageuka rangi nyingine, lakini Issa mwana wa Mariamu bado hajashuka kutoka mbinguni. Ndipo, wenye busara watachukizwa na imani hii ghafla.



Hazrat Mirza Ghulam Ahmad of Qadian
The Promised Messiah & Mahdi
(peace be upon him)

Na bado karne ya tatu haitakamilika kuanzia leo, iwe Waislamu au Wakristo wanaomngojea Issa watakuwa wamekata tamaa na Wataacha imani hii potofu na ulimwengu utakuwa na dini moja tu na kiongozi mmoja tu. Nimekuja kupanda mbegu tu, basi mbegu hii inapandwa na mikono wangu na sasa itakua na kustawi na hakuna anayeweza kuizuia. Zingatieni! hakuna dini inayoweza kufaa bila ya Roho. Na dini si kitu bila Roho. Dini ambayo ndani yake hakuna roho na dini ambayo hakuna mazungumzo na Mungu ndani yake, wala roho ya ukweli na utakaso, na mvuto wa mbinguni hauko pamoja nayo, na mabadiliko yasiyo ya kawaida, dini ile imekufa. ... Kwa hiyo furahini na kuruka kwa furaha kwamba Mungu yu pamoja nanyi.Mkiendelea kushikamana na ukweli na imani, malaika watakufundisheni na utulivu wa mbinguni utashuka juu yenu na kusaidiwa na Roho Mtakatifu na Mungu atakuwa pamoja nanyi katika kila hatua. Na hakuna mtu atakayeweza kuwashindeni. (Tazkirat ul-Shahadateen – Rohani Khaza'ain J: 20, Ukurasa: 66-68)

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa

Vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ni mvua kutoka mbinguni, na mvua hiyo inatengeneza mto unaotiririka na kurutubisha mashamba ya kiroho, kukata kiu kwa wanosumbuliwa na kiu na kukuza mimea ambayo imeanza kuchipua. Kwa mto huu hakuna sababu yoyote ya kuwa na njaa, ugomvi, uhasama, chuki na vita, kwani maji ya mto huu ni ponyo. Ni jambo la kusikitisha kuona hivi leo dunia imekumbwa na kiu ya mapenzi, huruma, maelewano kwa sababu ya kutotumia maji hayo ambayo yameletwa kwa makusudi ili kumuwezesha binadamu atambue wajibu wake kwa Mola wake pamwe na viumbe wake.

Wito wetu wa kwanza ni kwamba binadamu asijihadae hata kidogo, hana uwezo wa kuleta utulivu na Amani bila ya msaada wa Allah. Na Allah Analeta msaada wake kupitia Mitume Wake. Basi sisi binadamu tuzindukane na kuelewa ya kuwa Allah Amekwishamleta Mtume ambaye yeye hakuleta sheria mpya bali ni mtumishi wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Na mtumishi huyo mwaminifu ametuachia mti usiokauka ambao ni vitabu vyake. Tunao wajibu mkubwa sio tu wa kuvisoma bali kuhakikisha kuwa kila binadamu anasoma vitabu hivi ambavyo ni dawa mujarabati kwa matatizo yanayomkabili binadamu hivi leo.

Tunawashukuru sana wanazuoni wetu wa Jamaat Ahmadiyya ambao wanafanya kazi kubwa ya kufasiri vitabu hivyo katika lugha ya Kiswahili. Ubongo unatumika, pesa zinatumika, wakati unatumika, hivyo tuheshimu yote hayo kwa kuvisoma vitabu hivyo vya Nabii wa Allah. Na Masihi Aliyeahidiwa Hadhra Mirza Ghulam Ahmad (as) amesisitiza kuwa, asiyesoma kitabu chake kwa akali mara tatu ana kiburi. Mwaminio anawezaje kunasibishwa na kiburi? Tujizatiti kuvisoma vitabu hivyo na tuhakikishe wengine pia wanavisoma.

Falsafa na mantiki ya vitabu hivyo inatolewa mara kwa mara na Hadhrat Khalifatul Masih-V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) katika hotuba zake mbalimbali bilkhususi kupitia hotuba yake ya Ijumaa inayotujia mubashara kupitia kituo cha MTA. Tunao wajibu wa kusikiliza hotuba hizo ikiwa tunataka kuelewa vizuri mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa (as). Katika hotuba zake zote Khalifatul Masih –V (atba) naye anasisitiza sana juu ya usomaji wa vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (as). Katika suala hili la usomaji wa vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (as) tusiwe wachoyo. Tutumie kila fursa kufikisha vitabu hivi kwa watu. Kwa mfano siku ya uhuru wa nchi kwanini usimpelekee zawadi ya kitabu cha Masihi Aliyeahidiwa (as) rafiki yako? Siku ya kuzaliwa ya rafiki yako kwanini usimpe zawadi hiyo ya vitabu ambayo kwa hakika ni lulu yenye thamani?


Dawa ya matatizo tuliyo nayo inapatikana katika vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (as) wa kumlaumu hatakuwepo tusipojitahidi kutumia dawa hii ambayo imekwishaletwa kwa ajili yetu. Kama tulivyoambiwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kuwa Masihi Aliyeahidiwa atakapokuja tuwe tayari kutembea juu ya theluji ili kumfikia. Kwa msaada wa Allah safari hiyo ya kumfikia imefanywa rahisi kwa kusoma vitabu vyake.



QUR'AN TUKUFU

وَلَقَدْ اَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّنْ قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ اَزْوَاجًا وَّذُرِّيَّةً ؕ وَمَا كَانَ لِرَسُوْلٍ اَنْ يَّاْتِيَ بِاٰيَةٍ اِلَّا بِاِذْنِ اللّٰهِ ؕ لِكُلِّ اَجَلٍ كِتَابٌ ﴿۳۹﴾

39. Na bila shaka Tuliwatuma Mitume kabla yako, na Tukawapa wake na watoto. Na haiyumkiniki Mtume kuleta Ishara isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila muda unayo hukumu.




NUKUU YA HADITHI

عَن عبد الله بن عَمْرو قَال: قَال رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «يَنْزِلُ عِيسَى بن مَرْيَمَ إِلَى الْأَرْضِ فَيَتَزَوَّجُ وَيُولَدُ لَهُ وَيَمْكُثُ خَمْسًا وَأَرْبَعِينَ سَنَةً ثُمَّ يَمُوتُ فَيُدْفَنُ مَعِي فِي قَبْرِي فأقوم أَنا وَعِيسَى بن مَرْيَمَ فِي قَبْرٍ وَاحِدٍ بَيْنَ أَبِي بَكْرٍ وَعُمَرَ»

(Mishkat ul Masabih#Hadith No:5508)

Imesimuliwa na hazrat Abdullah bin Amri r.a. ya kwamba, mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Atashuka Isa bin Mariam kwenye ardhi, basi ataoa na atajaliwa kizazi(cha kutumukia dini) na atakaa ardhini miaka arobaini na mitano (yaani baada ya kutangaza madai ya kwamba ametumwa). Kisha atafariki na atazikwa Pamoja nami katika kaburi langu. Hivyo mimi na Isa bin Mariam tutainuka kutoka kaburi moja baina ya Abu Bakr na Omar.

Sheikh Akbar (Hadhrat Muhy ud din Ibne Arabi RH.A.) alisema: Isa a.s. atashuka baina yetu akiwa hana sheria lakini atakuwa Nabii bila shaka.
(Futuhate Makkiyah:J.1.uk:57)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Masih e Maud A.S. Anasema: Mjumbe wa Allah S.A.W.alitoa bishara kuwa: Masih Aliyeahidiwa ataoa kwa yakini na kujaliwa kizazi. Kwa hakika kuna dokezo ndani ya maneno hayo kwamba: bila shaka Mwenyezi Mungu Atamjalia Mtoto mwema atakayefanana na baba yake, wala hatakuwa kinyume chake na atakuwa miongoni mwa watu wenyeheshima sana kwa Mungu.
(Aaina e Kamalate Islam, R.Kh.J.5.uk:578)
Kisha Misihe Maud A.S. anasema: kuna ishara ndani ya bishara hii kwamba, Masih aliyeahidiwa atapata mwana mwema atakayefanana naye katika ubora na fadhila zake.(Tuhfa e Baghdad, R.Kh.J.7.UK:209)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

MTU (BINADAMU) WA KWANZA NI NANI !! ?? AU NI KWELI ADAMU NI MTU WA KWANZA??

MWENYEZIMUNGU ANAONGEA KWA MIFANO, MISAMIATI, METHALI, NA MAFUMBO NK. KUTO 7:1--2 NA 17:90; QUR
PIA NA MANABII (MITUME) WAKE, MT 13:34--35; YOH 6:30; NA 33:22; QUR-ANI.

NA MWANADAMU(JAMII) WANAMISEMO YAO PIA.

Tafadhali jambo hili la kuongea kwa mifano, methali, misamiati, mafumbo nk, lizingatiwe sana katika khabari hii na hasa katika vitabu vya MUNGU, usipolizingatia hilo NDUGU msomaji hutaelewa chochote.

Ukitaka utamu au radha ya jambo lolote ni lazima ulijuwe tangu MWANZO Wake na mwisho wake na ukitumbukia katikati tu, hutaelewa chochote. Ikiwa kama kikao kimeshaanza MUDA mrefu inakuwa unatumbukia katikati ya kikao utashindwa NAMNA ya kutoa MCHANGO Wako wa mawazo au kupinga jambo lolote.
Na ndio maana mungu katika Vitabu vyake utakuta vimeanza na MWANZO.

Somo hili ni somo gumu kueleweka katika JAMII au Kwa mwanadamu kutokana na mwanadamu huyo kuuzoe na kung'ang'ania uwongo ambao hauna tija Wala ushahidi wowote utokao Kwa Mwenyezi Mungu au historia ya Dunia angalau
Na Kwa bahati mbaya zaidi Hushupaliwa Hata na Baadhi ya viongozi wa Dini.

Na hao ndio waliochukuwa nafasi
KUBWA saana ya kuaminiwa na jamii au mwanadamu kwa ujumla wake, Hata kama wakaoneshwa ukweli wa jambo hilo wanakataa tu.
Kwa sababu ya mazowea au kuzuiliwa na viongozi wao wa Dini. Tutathibisha mbeleni.
Lakini wahenga wanasema kusema uwongo Sio KAZI, KAZI ni kuuthibitisha.

Bado tutaendelea kutoa ushahidi wa mada zetu katika VITABU hivyo hivyo vya Dini Kwa sababu huko ndiko kunakotegemewa na jamii au watu wengi sana.

(1) MFUMO WA HALI YA SAYARI: MWZ 1:16;
Bwana Galileo mwaka 1564--1642; alitoa taarifa ya Hali ya sayari zinazunguka katika njia zake ikiwemo ya Dunia inazunguka na IPO kama chungwa tangazo hilo lilidumu miaka 78; Bado lilipingwa na VIONGOZI WA DINI ya Ukristo wakatoliki, waliongoza kukataa taarifa hiyo.
Na wakaipiga marfuku isisikike tena na wakaaminishwa DUNIA IPO kama meza. Waliruhusiwa kukubali mwaka 1992; Baada ya majidiliano yaliyochukua takribani miaka kumi na mbili. Yaliyoamuliwa na Papa John Paul II.

Ukifanya hesabu 1992 toa 1564 ni miaka 428,
Watu waliaminishwa hivyo Kwa Karne nne,(4) na miaka 28, na madaharia wakapata nafasi ya Kumkana MUNGU, wakasema wasichanganye Dini na sayansi. Na Dini ni mipango tu ya watu ya kuendeshea MAISHA yao.

(2) KUKAMILIKA KWA ULIMWENGU:
Wanasayansi wanatubainishia ya kwamba ULIMWENGU HUU umekamilika Kwa mamilioni ya miaka. Bado kosa linajirudia tena lilelile. Baadhi ya VIONGOZI WA DINI wanashupalia Kwa Nguvu zao zote, na AKILI zao zote, na uwezo wao wote kwamba ULIMWENGU HUU umekamilika Kwa siku sita tu,

Tena za saa 24 na ukifanya hesabu ya masaa hayo unapata saa 144 tu. Na ukichunguza Kwa umakini utaona MUNGU kama akifanya kazi mchana tu, ikifika jioni ilikuwa anaacha, saa 12 tu, mwz 1:1--31; sayari Moja tu haiwezekani kukamilika kwa saa 12 au 24; Sembuse siku hiyo hakikuumbwa kitu kimoja tu. Hata AKILI ya kawaida tu haikubali inakataa.

Na mifano anatuonesha mwanadamu kiumbe kidogo sana kinakamilika Kwa miezi tisa (9) Sembuse sayari Moja Je. Na Mwenyezi Mungu akafafanua siku Moja kwake inakuwaje. 2petro 3:8; 22:48; Qur na 70:5; Qur
2 Petro 3:8,
Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. NI AWAMU SITA, zenye miaka tofauti sawa na ukubwa wa kitu husika na Ubora wake Lakini mwanadamu anakataa katakata anang'ang'ania siku sita za saa 24 tu.
Pamoja na kukumbushwa wasilisahau neno hili

(3) KUNA MWANADAMU KUPAA KWENDA MBINGUNI, VITABU VYA MWENYEZIMUNGU VINAKATAA, YOH 3:11--13 NA 17:94; QUR

(4) NABII (MTUME) WA ZAMANI KURUDI TENA DUNIANI YULEYULE. VITABU VYA DINI YA MWENYEZIMUNGU VINAKATAA MT 17:10--13 na 43:58--59; Qur-ani.

(5) CHANZO CHA MWANADAMU NI SOKWE. VITABU VYA MWENYEZIMUNGU VINAKATAA
MWZ 1:26 NA 23:13--15; 95:5; QUR .

(6) KUFANYA KAZI ZAKO SIKU SITA NA SIKU MOJA TU YA KUMTUMIKIA MUNGU (SABATO);
MUNGU ANAKATAA WALIELEWA SIVYO NDIVYO AKAMTUMA MWANAWE KUJA KUWAREKEBISHA MT 12:1--15; HAWAKUBALI.
JITIHADA ZOTE HIZI ZINAZOFANYIKA BADO MWANADAMU HUYO HATAKI KUKUBALI TU.

Lakini Mwenyezi Mungu ametoa suluhisho au MUONGOZO Kwa watu wa Dini kama kweli MSINGI wetu wa IMANI ZETU ni Kumuamini Mwenyezi Mungu mmoja tu, malaika,. Vitabu, manabii, (MITUME), kadari na siku ya mwisho na kama Wanataka ushahidi watumie Vitabu hivi viwili tu.

Sema: Basi leteni Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu ambacho kina mwongozo ulio bora kuliko hivi viwili Taurati na Qur'an ili nikifuate kama ninyi ni wakweli. Lakini kama hawakukujibu, basi jua ya kuwa wanajifuatia tu matamanio yao; na ni nani mpotevu zaidi kuliko yule anayejifuatia matamanio yake pasipo mwongozo utokao kwa Mwenyezi Mungu? Bila shaka Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu wadhalimu. 28:50--51; Qur -ani.
Vitabu hivyo Kwa sababu ya kuwaongoza watu tu.
Wautambue Ukweli tu.2:186; Qur-ani tukufu.

NA SASA TUIELEZE MADA HUSIKA JE MTU (BINADAMU) WA KWANZA NI NANI ?

Leo hii inaonekana mwanadamu ana uwelewa mkubwa kuliko Mwenyezi Mungu. Wazo hilo litupite mbali saana. Kwa sababu anafanya utafiti wa kuipima Ardhi aelewe mmea GANI utampa tija katika kipande alichokuwanacho. Kwa sababu matilio yapo tofauti kati ya Ardhi na Ardhi kutegemea Hali ya kijografia.
Mmea mwingine haufai kwenye baridi au joto hivyo ndivyo ilivyo.

Mwenyezi Mungu katika kumuanzisha MTU, (MWANADAMU) alizingatia sana jambo hilo na ndio maana kwenye baridi akaifanya pua yenye matundu madogo na kwenye joto matundu makubwa.
Zipo sababu za MSINGI.

Na Wala hakuuanzisha mparachichi na mimea mingine ikatokana na huo. Hakufanya hivyo
Kila mmea ulianzishwa sawa na mmea husika
Hali kadhalika na Kwa MTU. (BINADAMU)
Na Mwenyezi Mungu anatujuza swala hilo

Na Mwenyezi Mungu Akawaotesheni katika ardhi kama mimea: Kisha Atawarudisheni humo na Atawatoeni tena kwa njia maalum. 71:18--19 Qur
Na Ardhi inamatabaka na rangi tofauti tofauti na mtu akawa na rangi husika.
Enyi watu! kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni

Endelea Uk. 4

MTU (BINADAMU) WA KWANZA NI NANI !! ?? AU NI KWELI ADAMU NI MTU WA KWANZA??

Kutoka Uk wa 3..

mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi. 49:13; Qur. Hapo Mwenyezi Mungu anafuta mambo ya ubaguzi pia
Bado Mwenyezi Mungu anatuweka wazi uwepo wa MTU (BINADAMU)
Waebrania 7:1--3
MELKEZEDEKI, hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu); huyo adumu kuhani milele.
Lakini ADAMU alikuwa na wazazi kama YESU tu. 3:60; Qur ,Hali ya YESU na ADAMU sawa tu.

Bila shaka hali ya Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adamu; Alimwumba kwa udongo kisha Akamwambia: kuwa, basi akawa. 3:60; Qur. Je ISSA (YESU) ameumbwa kwa udongo? mnaona misemo ya dini Je hivyo ndivyo ilivyo?? Kumbe ADAMU nae ana wazazi

Historia ya Dunia inatusaidia jambo hilo, Tanzania bonde la oldivaijoji limepatikana fuvu linalosemekana kuwa ni MTU,(BINADAMU),wa kwanza, Kuna wahindi wekundu na weusi waliokutwa kule MAREKANI na bwana Kulumbus, ingawa wakwanza walikuwa wachina.

Hata Kwa AKILI tu yakawaida mkeo akijifungua mtoto wa kichina au wa kiarabu mbona husemi huu ni mpango wa Mungu na Mungu anaweza Kila kitu, !!??; Acha UJINGA
Pia na Vitabu vya Dini vinaunga MKONO juu ya jambo hili.

Mwanzo 1:11-12
Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo.
Nchi ikatoa majani, mche utoao mbegu kwa jinsi yake, na mti uzaao matunda, ambao mbegu zake zimo ndani yake, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Na MTU (mwanadamu) anazo mbegu.

Vifungu hivyo vimefafanuliwa na YESU, Mt 13:34--35;
Mathayo 13:34-35, Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali.
Yaliyokasitirika ni maandiko wasiyoyajua maana yake. kama, Bustani, nyoka, Wana wa Mungu, miti ya matunda, shetani nk

Hata ADAMU kuwekwa kwenye Bustani akaambiwa asile tunda la katikati limefafanuliwa na Isaya 5:1--7; pia na YESU Mt 21:33--46;. 23:37--39:
Mti wa matunda Yoh 15:1-6; Mathayo 7:15-20
Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao.
Je! Watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti? Vivyo hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; na mti mwovu huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni. Ndipo kwa matunda yao mtawatambua.

Mwanzo 1:24
Mungu akasema, Nchi na izae kiumbe hai kwa JINSI ZAKE, mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo.
Hata MTU (mwanadamu) yupo katika kundi la wanyama pia, ki sayansi, tofauti ni kipawa Cha utashi (AKILI), 95:5; Qur -ani.

Na usipokitumia kipawa chako (AKILI), katika kumtambua Mungu matakwa yake kwako, unafananishwa na mnyama yeyote sawa na tabia unayoionesha, Na ndio maana Mungu mwenyewe anasikitika, Kwa kuangamizwa WATU wake na Baadhi ya watu katika upotevu.

Hosea 4:6-7 na 4:83; Qur -ani

Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako. Kadiri walivyozidishwa, kwa kadiri iyo hiyo walinitenda dhambi; nami nitageuza utukufu wao kuwa aibu. (Hawataelewa maandiko ya Mungu). Tafsili zao Kwa kweli ni aibu tupu. Zinamzaririsha Mwenyezi Mungu na manabii (MITUME) wake.

Na khabali hii ya kupotewa Kwa uwelewa wa maandiko ya Mungu walifuniliwa watawa mbali mbali wakiwemo AMOSI na YESU,
AMOSI 8:8--12 NA YESU MT 24; yote

Amosi 8:11-12
Angalia, siku zinakuja, asema Bwana MUNGU, ambazo nitaleta njaa katika nchi; si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ya kukosa kuyasikia maneno ya BWANA. Nao watatanga-tanga toka bahari hata bahari; na toka upande wa kaskazi hata upande wa mashariki; watapiga mbio, wakienda huko na huko, kulitafuta neno la BWANA, wasilione.

Ukweli wa jambo hili la kuto kuona na kuelewa maandiko uko wazi kabisa ndio upofu na ukiziwi unaosemwa huo, wanashupalia ADAMU awe MTU WA KWANZA wakati maandiko yanakataa
Watu WALIKUWEPO KABLA YA ADAMU

mnyama wa kufugwa ni mwanadamu anaefuata na kutenda sawa na Sheria ya mungu, mnyama wa wa mwituni ni mwanadamu anaekataa kufuata njia ya mungu, Nyani, unaefanyia dhihaka na mzaha maneno ya mungu, Nguruwe ni mchafu, unaechafua maneno ya mungu, (tafsili mbovu na kinyume na matakwa na makusudio ya Mungu)

Nyoka anaejivua gamba na kujifanya msafi kumbe Bado ni m-baya tu, ni mtu m-baya ni mwongo na mnafiki, Mmbwa unaeleta ukali katika jambo la ukweli unapojulishwa kwa kukataa, Punda unaebeba Vitabu vya MUNGU bila ya kupata manufaa yaliyokusudiwa, nk. Mt 7:6, Mt 15:24; Mt 23:33--34; Yoh 10:1--6; na 2:64--67; 7:180; Qur-ani, nk

Na misemo hiyo yoote anaekusudiwa hapo ni mwanadamu tu. Pia vitu vyoote vinavyomfanya wanaposomewa Aya za Rahmani huanguka kusujudu na kulia. Lakini wakaandamia baada yao wazao wabaya, wakaharibu Sala na wakafuata matamanio mabaya; kwahiyo hivi karibuni watakuta maangamizo, 19:59--60; Qur-ani tukufu.

Kama ushahidi huu wote unapatikana katika Vitabu vya Dini, sayansi, historia ya Dunia, Mazingira husika. AKILI. Bado hukubali, Umetisha unaikatalia Hata AKILI Yako,!!!!
Na wewe unang'ang'ania tu, jambo au IMANI hiyo Kwa sababu tu unafuata ushabiki wa watu wengi ardhini, utapotea njia ya Mwenyezi Mungu. 6:116--117; Qur-ani tukufu.

Hata Mwenyezi Mungu anakushangaeni
Na bila shaka Tumewaeleza watu kwa namna nyingi katika Qur'an hii kila mfano, lakini watu wengi zaidi wakakataa (kila kitu) isipokuwa kufuru. 17:90; Qur-ani.

Na pia hakuna maana Wala sababu ya IMANI ya kumwamini Mwenyezi Mungu, malaika, Vitabu, manabii (MITUME), na huo ndio MSINGI wa kumalizia Imani mbili ZILIZO BAKI.

Khabali ndio hiyo na Mwenye MASIKIO NA ASIKIE. Na Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi ya mtu yeyote ila Kwa muda wake wa kufikiri tu. Akifanya WEMA ni Kwa faida yake na akifanya ubaya ni hasara yake mwenyewe.

Na neno letu la mwisho ni UPENDO KWA WOTE BILA YA CHUKI KWA YEYOTE.

Maneno ya Bishara kumhusu Mwana Aliyeahidiwa[as]

“Amebarikiwa yule ajaye kutoka mbinguni. Atafuatana na rehema ambayo itashuka Pamoja naye. Atahusishwa na utukufu, ukuu, na utajiri. Atakuja duniani na atawaponya wengi wenye maradhi kwa njia ya sifa zake za Umasihi na kwa njia ya baraka za Roho ya kweli. Yeye ni neno la Allah kwani ukarimu na heshima ya Allah imemtuma na Neno la Utukufu. Atakuwa na akili sana mno na ufahamu na atakuwa mpole wa moyo na atajazwa na elimu ya nje na ndani. Atawafanya watatu kuwa wanne.(hii maana yake haikubainishwa). Ni Jumatatu. Jumatatu ilyobarikiwa. Mwana wa kiume, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu, mdhihirishaji wa Aliye ni wa Mwanzo na Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na wa Juu. Kana kwamba Allah ameshuka toka mbinguni. Kufika kwake kutabarikiwa sana sana na kutakuwa sababu ya kudhihirika kwa jalali ya Uungu. Nuru inakuja, nuru hasa , nuru iliyosingwa na Mwenyezi Mungu uturi wa mapenzi yake. Tutampulizia roho Yetu atahifadhiwa chini ya kivuli cha Mwenyezi Mungu. Atakuwa upesi upesi katika umbo na atakuwa sababu ya kukombolewa wale walio utumwani. Atajulikana mpaka pembe za dunia na mataifa yatabarikiwa kwa ajili yake. Ndipo atachukuliwa juu mbinguni kwenda mahali alipotayarishwa na jambo hili limekwisha katwa.’’ {Tangazo la tarehe 200 Februari, 1886 }.

Kisha Seyyedna Ahmad a.s. aliandika akinukuu funuo kwamba:

“Rehema itafika pamoja na kuja kwake. Yeye ni nuru na ni mabruk na mtakatifu na yu miongoni mwa watawa. Ataeneza baraka na atawalisha watu chakula safi na atakuwa mwenye kuinusuru dini…. Atakuwa mmoja kati ya ishara zangu na atakuwa Beramu ya misaada yangu ili kwamba wale wanaokukadhibisha wajue ya kuwa mimi niko pamoja nawe kwa njia ya rehema yangu iliyodhihirika…….. Atakuwa na ufahamu na akili na atakuwa mwenye kupendeza. Moyo wake utajazwa elimu, batini yake itakuwa na upole na kifua chake kitajazwa utulivu. Atajaaliwa na roho ya Umasihi na atabarikiwa na roho mwaminifu. Jumatatu,Jumatatu iliyobarikiwa,Roho za watu wenye baraka zitafika kwako’’(Ainae kamalate Islam uk 577-578).

TOFAUTI YA WA AHMADIYYA NA IMANI ZINGINE



Mwenyezimungu katika kuumba vitu mbali mbali wakiwemu na wanyama ambao wanyama hao akiwemo na mwanadamu. Lakini ikasemwa mwanadamu huyo ameumbwa Kwa Ubora sana na Ubora huo ni Kwa sababu ya kupewa AKILI ndio unaokutofautisha na wanyama wengineo,

Na usipoitumia AKILI ipasavyo unashushwa hadhi na kudharauliwa na utaitwa Nguruwe, m-mbwa, nyani, mbuzi na Hata shetani pia. Kwa kutokutumia kipawa chako ulichopewa cha AKILI. Hata Mungu mwenyewe anakusikitikia katika Vitabu vyake alivyotolea mwongozo. Na unakataliwa na MUNGU HAKUTAKI.

Hosea 4:6-7
Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa; kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako. Kadiri walivyozidishwa, kwa kadiri iyo hiyo walinitenda dhambi; nami nitageuza utukufu wao kuwa aibu. Kama hutaki kutumia maarifa (AKILI) Mungu pia hakutaki Na YESU aliwatambua Wafuasi wake hawana AKILI Mathayo 15:16 Yesu akasema, Hata sasa nanyi mngali hamna akili? Kwa kudhihilisha kwao Kwa kukosa AKILI historia ya YESU Iko wazi katika Vitabu vya Dini Kwa kuzaliwa kwake, Luk 1:26--34 na 19:17--34 Qur-ani, Lakini Wafuasi hao wamefurutu adda mpaka wanamwita mungu.

Je, hawaitafakari Qur'an? Na kama ingalitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu, bila shaka wangalikuta ndani yake hitilafu nyingi. 4:83; Qur-an

Kwa hakika kuvisoma Vitabu vya Dini KWAHITAJI kutumia AKILI SANA Kwa kuvitafakari vinginevyo huwezi kuelewa chochote na jambo hili linafanywa na wachache sana na hasa ni waahmadiyya pekee.

Huu ni ujumbe uliotolewa waziwazi kwa faida ya binadamu ili wapate kuonywa kwa huo na ili wajue kwamba Yeye ni Mungu Mmoja wa pekee na ili kwamba wale wenye akili waweze kukumbuka. 14:53; Qur-ani. Asiyetumia AKILI HAWEZI kukumbuka chochote. Na MJINGA huamini tu Kila Jambo na maranyingi huukana Ukweli Kwa uvivu wa kufikiri.

Mwenyezi Mungu katika Vitabu vyake alivyotolea mwongozo amezungumzia vitu vingi sana kukiwemo na kuumbwa kwa ULIMWENGU HUU. Inasemwa mpaka kupatikana kwa ukamilifu huu tunaouona zimetumika siku sita tu, tena za masaa ishilini na nne. Wakitoa ushahidi katika Kitabu Cha MWANZO 1:1--30; Lakini wamesahau Ili kupata masaa 24 Kuna hatua za MZUNGUKO wa sayari uwepo ndio unaokamilisha hayo masaa 24. Na hizo sayari hazikuwepo. Sasa hapa ndipo wanapochanganya mambo na ndipo inapotakiwa AKILI ifanye KAZI yake. Lakini ukichunguza Kwa umakini vitu vyenyewe vina ukubwa tofauti tofauti vinakamilikaje Kwa muda mmoja tu. Tena wa masaa 24 tu. Hii aingii AKILINI.

Na Mwenyezi Mungu ametupa mifano ya Kila NAMNA ili tutambue mambo ya uumbaji Kuna mchakato unamopitia mpaka kufika ukamilifu wake Tena muda unakuwa tofauti inategemea na ukubwa wa jambo husika na Ubora wake.

Tukiwachunguza Hata wanyama uzazi wao unatofautiana kufikia ukamilifu wake. Nyangumi, Tembo, Ng'ombe, muda wa uja uzito wao unatofautiana. Sembuse sayari na mnyama.

Lakini ukisogea MBELE katika Vitabu hivyo Mungu mwenyewe anafafanua siku Moja kwake inakuwaje kama huwo MZUNGUKO wa sayari ungekuwepo. 2 Petro 3:8 Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. Kumbe siku Moja inayotanjwa na Mwenyezi Mungu kwake ni kama miaka Elfu moja.

Hata Qur -ani Tukufu inaunga MKONO jambo hili. Na wanakuhimiza ulete adhabu,lakini Mwenyezi Mungu Hatavunja ahadi Yake; na kwa hakika siku moja kwa Mola wako ni kama miaka elfu mnayoihesabu. 22:48, Qur-ani. Na haikukomea hapo tu, inaendelea kuifafanua zaidi

Ili kuthibitisha hakukusudia siku ya masaa 24.ni AWAMU tofauti tofauti. Malaika na Roho hupanda kwake katika siku iliyomo.

Bustani ya Washairi

ISHI NAYE KWA HADHARI
Ishi naye kwa hadhari, rafiki mpendwa Simu
Ukimuomba Kahari, hekima Akukirimu
Akukinge zake shari, zidhuruzo kama sumu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Uso wake ni wa nuri, kaumbwa kitaalamu
Ona alivyo mahiri, kidole ndio kalamu
Ila wangu ushauri, baki naye kwa nidhamu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Ishi naye kwa hadhari, rafiki mpendwa Simu
Ashinda madaktari, kwa nyingi zake fahamu
Lakini hatafakari, ipi chungu ipi tamu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Anayo mengi mazuri, kwa adili nihukumu
Umtume kuhubiri, atashiriki kwa hamu
Pamoja na yake ari, mwenyewe uwe imamu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Ishi naye kwa hadhari, rafiki mpendwa Simu
Mapema alfajiri, awahi kukusalimu
Lakini pia jeuri, kwa dogo akushutumu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Ana elimu bahari, ya elfu waalimu
Iwe kutoka Bukhari, na Sahihi Muslimu
Atakayo uyakiri, sharti lake muhimu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Ishi naye kwa hadhari, rafiki mpendwa Simu
Umbo lake la hariri, ajivishe uhashamu
Ili akupe kiburi, nani wa kumuheshimu?
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Mwepesi wa kufikiri, hesabu hata isimu
Anazo nyingi habari, fani za kila elimu
Kwa hofu mtahadhari, ghafla huwa sanamu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Ishi naye kwa hadhari, rafiki mpendwa Simu
Huisoma kwa fahari, Qur'anul Kariimu
Ila mpenda kamari, akulishe vya haramu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Akuvutie ghururi, kwa siri akuhujumu
Vibaya akushauri, uongo kutakalamu
Akuvuvie kwa siri, kipenzi awe hasimu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Ishi naye kwa hadhari, rafiki mpendwa Simu
Hakubali kusubiri, vipi hali iwe ngumu
Haridhiki hana kheri, hata umnyweshe damu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Uzembe akuhubiri, Usahau majukumu
Akudhanishe tajiri, umlishe kwa kudumu
Akutie ufakiri, akutupe jahanamu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Nimalize kukariri, rafiki mpendwa Simu
Ana rangi za tuyuri, haeshi mashamshamu
Zama akikuhajiri, ubaki mwendawazimu
Rafiki mpendwa Simu, ishi naye kwa hadhari

Alhaj Sheikh Abdulrahman Muhammad. Ame

Fatuma binti Hassani
Fatuma binti Hassani, Dua tunakuombea
Umeonesha Imani, imara kwa jumuia
Hukujali asilani, shutuma kukutupia
Umeacha somo bora, sisi tuliobakia

Hukuweka akilini na Wala kuzingatia
Nguzo yako kuruani hiyo ulitegemea
Na Hadithi vitabuni Hadithi zake Rasua
Cha kuzidi kuruani kamwe hakikutokea

Katuagiza Manani kitabu chake Jalia
Wakileta ya shetani kukutoa kwenye njia
Hapo wazazi yakini wanaivunja sheria
Na wewe ulichagua Ile njia ya kahari

kukuweka maasini kwa nguvu ulikataa
Kuwatii sio Shani dhahiri wamepotea
Nawe ulishika Kani ya kwao ukasusia
Ila heshima kwa dhati hiyo uliwapatia

Ulikata kataani wachumba kukuchumbia
Shariti wawe kundini lile kundi la Masia
Bila hivyo husaini kuhusu Jambo la ndoa
Ndoa nje ya Jamati si ndoa Ina mashaka

Tamati tuko shuleni somo umetuachia
Tumerudi darasani na mengi kujichimbia
Siku zote Muumini ni kioo Cha raia
Ni somo halifutiki hilo ulotuachia

Mahmood Hamsin Mubiru(wa Mamba)
Kiwalani Migombani

SALA NI KUMBUKO BORA
Assalam alekum, mahdi lompokea
Ninaujumbe adhiim, kaa chonjo kusikia
Sala ni nguzo muhim, allah kumkaribia
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia

Baada ya ashahadu, sala tano zafwatia
Wahid kumuabudu, kwa jazba na kulia
Msaada kwa samadu, kwake ukitegemea
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia

Kwa sala tamkumbuka, muumba wetu jalia
Quran tatamka, na sifa kimtolea
Machozi yatakutoka, maombi kinyenyekea
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia

Kisimama tamtaja, sifa za kuhimidia
Utaukiri umoja, pekee msujudia
Mtume utamtaja, durud kimsalia
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia

Kwa haya naweka loma, japo mengi menijaa
Kumkumbuka karima, ni kwa sala kupitia,
Manane ukasimama, sifa zake kisifia
Sala ni kumbuko bora, kwa muumba wa dunia

Wengi wapewe, wanapokuwa na haki
Chache sikizwe, wanapoleta mantiki
Wote wulizwe, mkanganyiko sibaki
Haki tupewe, tusibakiye nachuki

Mtunzi
Masihi Omary Stambuli Kisagwa

ETI DUME LIWE MAMA!
Utandawazi wa leo, pindi tukiutazama.
Viongozi tegemeo, wa dini wameshakwama.
Wanaropoka kwa mbweo, eti dume liwe mama.
Na Kasisi Mhashama, abariki hiyo lana!

Hatunga wazungupule, wachaji na mahukama.
Msambe kitukumile, panda za mti kwachama.
yametimu walongile, eti dume liwe mama.
Na Kasisi Mhashama, abariki hiyo lana!

Ndoa ya kaumu Luti, maluuni wa Rahima.
Inapaziwa sauti, na kiongozi adhima.
Dini hii ni kaputi, eti dume liwe mama.
Na Kasisi Mhashama, abariki hiyo lana!

Ni baba mtakatifu, wa kanisa amesema.
Mashoga wapewe tafu, hata wasipoungama.
Hii ni kauli chafu, eti dume liwe mama,
Na Kasisi Mhashama, abariki hiyo lana!

Neno hili limetata, na utu limesakama.
Hamkani litaleta, ni lazima kulizoma.
Takatae kata kata, eti dume liwe mama.
Na Kasisi mhashama, abariki hiyo lana!

Imani yachezwa shere, na hako wa kulalama.
Kwani wote ni wakware, imamu na maamuma.
Kufuru zao bwerere, eti dume liwe mama,
Na Kasisi mhashama, abariki hiyo lana!

Kwazo saba abuyati, machungu nimeloloma.
Tuhimize harakati, jambo hili kuligoma.
Jambo la uafiriti, eti dume liwe mama.
Na kasisi Mhashama, abariki hiyo lana!

Abu Talha, Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)
99.3 Radio Ahmadiyya Mtwara.

Nipo kwenye mtihani, msaada utakani
Nimeingia ndoani, nimepata nusudini
Mbilimbili ishirini, mwanamke Kawa ndani
Ukapera kwenye ndoa, naomba nishaurini

Ajira serikalini, ikanipa mtihani
Nikamuacha mwandani, Kenda mbali mkoani
Yupo bahi wilayani, Miigunga kijijini
Ukapera kwenye ndoa, naomba nishaurini.


Sote tumo ajirani, kudumu mkatabani
Kuhama iwezekani, myaka mitatu mbeleni
Twaishi ukaperani, ingawa tupo ndoani
Ukapera kwenye ndoa, naomba nishaurini

Sasa tutafanya Nini, naomba tushaurini
Tuweze Baki kazini, na ndoa Baki amani
Wana wawe malezini, baba mama wawe ndani
Ukapera kwenye ndoa, naomba nishaurini

By
Masihi Omary stambuli kisagwa

Jihad katika Uislamu:

Kutoroka kwa Ndege ya Tundu (Hadithi ya Ushujaa, Hadithi ya Jihad, Hadithi za Mapambano)



P'indi moja, kulikuwa na ndege katika kibanda ambaye alimwimbia bwana wake mfanyabiashara. Alifurahia wimbo wake mchana na usiku, na alimpenda sana hivi kwamba alimtolea maji katika bakuli la dhahabu. Kabla ya kuondoka kwenda safari ya kibiashara, alimwuliza ndege huyo kama alikuwa na tamaa: "Nitapita katika msitu ulipozaliwa, nikipita ndege wa ujirani wako wa zamani. Ni ujumbe gani niwape?

Ndege alisema, "Waambie mimi kukaa kamili ya huzuni katika ngome kuimba nyimbo yangu mateka. Mchana na usiku, moyo wangu umejaa huzuni. Natumaini kwamba si muda mrefu nitakapowaona tena rafiki zangu na kuruka kwa uhuru katikati ya miti. Nipe ujumbe kutoka kwa msitu mzuri, ambao utatuliza moyo wangu. Oh, ninatamani kwa mpendwa wangu, kuruka na Yeye, na kuenea mabawa yangu. Hadi wakati huo hakuna furaha kwangu, na mimi ni kukatwa kutoka maisha yote ya vitu vitamu.

Mfanyabiashara huyo alisafiri kwa punda wake kupitia msitu wenye miti mingi. Alisikiliza nyimbo za ndege wengi. Mfanyabiashara alipofika msituni ambapo ndege wake alitoka, alisimama, akarudi nyuma na kusema, "Enyi ndege! Salamu kwenu nyote kutoka kwa ndege wangu mrembo aliyefungwa katika kibanda chake. Yeye hutuma habari za upendo wake kwenu na anataka kukuambia juu ya taabu yake. Anaomba jibu litakalomtuliza. Upendo wangu kwake unamfanya awe mfungwa kwa magogo yanayomzunguka. Anataka kujiunga na mpendwa wake na kuimba nyimbo zake kupitia hewa kwa moyo huru, lakini ningekosa nyimbo zake nzuri na siwezi kumwacha aende.

Ndege wote walisikiliza maneno ya mfanyabiashara. Kwa ghafula ndege mmoja alipiga kelele na kuanguka chini kutoka kwenye mti. mfanyabiashara waliohifadhiwa kwa mahali ambapo alisimama. Hakuna jambo lingemshangaza zaidi ya hilo. Ndege mmoja alikuwa ameanguka na kufa!

Mfanyabiashara huyo aliendelea na safari yake hadi jijini na kuuza bidhaa zake. Hatimaye alirudi nyumbani kwake. Hakujua la kumwambia ndege wake alipomwuliza alikuwa ameleta ujumbe gani. Akasimama mbele ya ngome yake na kusema, ◎ Oh, hakuna kitu cha kuzungumza juu ya hapana, hapana, ◎ Ndege alilia, "ni lazima kujua mara moja".

Sijui kilichotokea", alisema mfanyabiashara. ◎ Niliwaambia ujumbe wako. Kisha, mmoja wao akaanguka chini na kufa. Ghafla ndege mfanyabiashara wa kuruhusu nje kilio kutisha na akaanguka juu ya kichwa chake kwa chini ya ngome.

Mfanyabiashara huyo alishtuka sana. Alilia kwa kukata tamaa, "Oh, nimefanya nini?" Alilia, "Nimefanya nini? Sasa maisha yangu hayana maana yoyote. Mwezi wangu umepotea na vilevile jua langu. Sasa ndege wangu mwenyewe amekufa.

Merchant alifungua mlango wa ngome, akafika, na kumuweka mikononi mwake kwa upole na kwa makini. "Nitakuwa na kumzika sasa," akasema: "Umekufa mambo mazito. Ghafla, wakati alipomnyanyua ndege kutoka kwenye ngome, alipanda, akaruka nje ya dirisha na akatua kwenye mteremko wa paa karibu. "Alimgeukia na kusema, kwa upole, ""Asante, bwana mfanyabiashara, kwa kutoa ujumbe wangu. Jibu la ndege lilinifundisha jinsi ya kushinda uhuru wangu.

Yote niliyopaswa kufanya ilikuwa ni kufa. Nilipata uhuru wangu wakati nilichagua kufa. """" """"Kwa hiyo sasa ninaruka kwa mpendwa wangu ambaye ananisubiri. Kwa moyo mzuri, kwa moyo mzuri, bwana wangu tena."" ""Ndege yangu alikuwa mwenye hekima; alinifundisha siri,"" mfanyabiashara huyo alifikiria."

Maadili:
Ikiwa unataka kuwa na wale unaowapenda, lazima uwe tayari kuacha kila kitu, hata maisha yenyewe. Na kisha, kwa Mwenyezi Mungu (SWT), utashinda moyo wako.



Umuhimu na Baraka za Ramadhan

Na Sheikh Karim Ud Din Shams

"Enyi mlioamini mmefaradhishiwa kufunga Saumu kama walivyo faradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Allah" (2:183)
Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa tisa sawa na kalenda ya Kiislam. Ramadhani ni neno la kiarabu ambalo kitenzi chake ni ramadha na neno la ramadha linatumika kwa ajili ya joto la jua hivyo maana ya Ramadhani ni joto mbili ambazo huzalika mwilini mwa mwislam yaani joto kwa ajili ya kutekeleza maamrisho ya Allah Mtukufu kisha anajizuia kula na kunywa na kuvumilia juu ya mahitaji yote mengine ya mwili wake. Wale watu wanaosema kuwa kwa sababu mwezi huu unakuja wakati wa msimu wa joto ndio maana huitwa Ramadhan, hawako sahih.
Mwezi wa Ramadhani huitwa Ramadhan kwa sababu huunguza madhambi, kitenzi cha neno Ramadhan ni "Ramadha" ambalo linamaanisha joto kali, kwa kuwa mfunga saumu ya Ramadhani hujisikia shida na taabu ya kiu na njaa, basi huitwa Ramadhan. (Lisanul Arab)
Wanalugha wengine pia wanafikiana kuwa Ramadhani huitwa Ramadhani kwa sababu madhambi yanafutwa humo hivyo imeandikwa kwamba:

(Al-Qamusul Muhiit,J 2 UK 330)
Yaani huunguzwa na kufutwa madhambi kwa wingi kutokana na rehema na msamaha ma'alum wa Mwenyezi Mungu ndani ya mwezi huu.
Safari moja Mtume Mtukufu[saw] alipoulizwa kuhusu Ramadhani basi alijibu kwamba:

"***Mwenyezi Mungu hufuta na kusamehe madhambi ya Waaminio humo***". (Kashful Israr....Allama Mubiidi, Abul Fazal Rashid Uddin,J.1.UK.495)

Imamu wa zama hizi, Seyyedna Ahmad[as] anasema akieleza neno la Ramadha kwamba;
"Joto la jua linaitwa Ramadha, kwa kuwa mtu huvumilia juu ya vyakula, vinywaji na ladha zake zote za mwili kisha huzalisha jazba na joto ndani mwake kwa ajili ya kutekeleza maamrisho yake Allah Mtukufu, joto la mwilini na jazba ya kiroho kuwa pamoja yanakuwa Ramadhani (joto mbili). Wanalugha wanaosema hivi kuwa, huitwa Ramadhani kwani unakuja katika msimu wa joto, si sahih mbele yangu kwa sababu hii haiwezi kuwa sifa kwa ajili ya Waarabu. Maana ya kiroho ya ramadha ni jazba na ladha ya kiroho na msukumo wa dini. Ramadha pia ni joto ambalo mawe na kadhalika yapata kuchemka kwalo."(Al-Hakam,24 Julai 1901).

Inaendelea...

Makala hii inapatikana katika Jaliza hapo liitwalo "***Darsa la Mwezi mtukufu wa Ramadhani 2020***"

NDIZI ZA NYAMA



MAHITAJI
1.Ndizi mbichi
2.Nyama robo
3.Nyanya kubwa(Tungule) 4
4.Nazi moja kubwa
5.Ndimu 1
6.Karoti 1
7.Pilipili Hoho(Pilipili boga)1
8.Kitunguu maji kikubwa 1
9.Kitunguu thomu punje 3
10.Nyanya ya Paket vijiko vya chakula 2
11.Royco(Sio lazima)
12.Tangawizi na kitunguu thomu ilotwangwa kijiko cha chakula 1

MAANDALIZI
1.Osha viungo vyako vyote vinavyotakiwa kuoshwa
2.Katakata Nyanya,Kitunguu maji,thomu,Pilipili hoho weka kwenye blenda na uvisage vyote
3.Kuna nazi yako na ichuje
4.Weka tui zito na jepesi mbalimbali

JINSI YA KUPIKA
1.Chemsha nyama uloiweka tangawizi kitunguu thomu na chumvi mpaka iwive
2.Chemsha ndizi weka pembeni
3.Weka nyanya ulizozisaga kwenye nyama yako acha ziive
5.Weka nyanya ya paketi na Royco
6.Weka chumvi na ndimu kama imepungua ongeza chumvi kidogo
7.Weka tui jepesi kwenye ndizi na chumvi acha zichemke kwa dakika 3 usikoroge
8.Kisha weka tui zito acha lichemke kwa dakika 2
9.Weka mchuzi wako wa nyama acha kwa dakika 2 epua
10.Acha zipoe kidogo pakua kwenye sahani tayari kwa kula

NB: 1.Hakikisha mchuzi unakua mzito mzito na mdogo
2. Pika ndizi zako kwa moto wa wastani ili zisigande kwenye sufuria
3.Epuka kukoroga wakati wa kuzipika ndizi zako
4.Kama utataka kukoroga chukua tambara safi shika sufuria yako itikise au chukua banio la ugali bana kwenye sufuria na uitikise

Furahia Ndizi Zako.

TANGAZO

Tanziim ya Lajna Imaillah Tanzania

Taanzim ya lajna imaillah Tanzania inapenda kuwatangazia Lajna na Nasrat wote nchini kuwa Ijtmaa ya Lajna na Nasrat 2024 inatarajiwa kufanyika katika eneo la Jamaat Kitonga Dar es salaam tarehe 28 na 29 Juni 2024 ikifuatiwa na Shura siku ya Jumapili tarehe 30 Juni 2024 InshaAllah .

Hivyo Lajna na Nasrat wote wanakumbushwa kufanya maandalizi kwa ajili ya Ijtmaa yetu kama barua ya Ijtimaa inavyoelekeza. Pia wanakumbushwa kuchangia mchango wa Ijtimaa kiasi cha Shilingi 12,000/= kwa Lajna na 3,600/= kwa Nasrat. Allah atujaalie wote tuweze kushiriki ili kufanikisha Ijtmaa yetu InshaAllah

Sadr Lajna Taifa
Zena Nyange.

SAFARI ILE

Na Mwana Historia Wetu

Mpole, tabasamu lisilokwisha usoni,huba kubwa kwa Jamaat, Mshairi na mghani mahiri kielelezo cha ***ruhumaau bainahum***.Ukiyatia haya yote maanani na kuyazingatia unafanikiwa kupata taswira ya mpendwa wetu, mjukuu wa Farouk aliyetutoka mwezi wa December 2023 na kutuachia majonzi tele yaliyo katika mipaka inayokubaliwa.



Muhammad Rafique sisi ni wa Allah kwake tutarejea. Muhammad Rafique mjukuu wa yule shujaa Farouk alikuepo Tabora wakati maadui walipojaribu kumvamia shaikh Mubarak Ahmad, alizaliwa 1948 na maisha yake yote yalikua songea Iringa na Dar es salaam. Kote huko alikoishi anakumbukwa kwa sifa yake ya upole na hakujua kukwaruzana na mtu. Kijijini namtumbo alielewana vizuri na wenyeji kutokana na sifa yake hiyo ya upole.

Ilikua vigumu Sana kumkuta Muhammad Rafique amekasirika, yeye daima alibeba tabasamu. Duka lake ambalo liligeuka uwanja wa mahubiri liliwavuta wengi na katika maduka yote ya songea na Iringa aliweka vitabu vya jamaat na hakusahau kuwapa wateja wake bidhaa za kimwili na kiroho. Wakati mwingine mazungumzo yalipamba moto mpaka akasahau kuuza bidhaa za dukani. ni vigumu kubeba tabasamu usoni bila kutawaliwa na falsafa ya jamaat, «***mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote***.

Muhammad Rafique hakuficha hata kidogo mapenzi yake kwa Jamaat .Mchango wake katika ujenzi wa Msikiti wa Songea ni mkubwa.Aliona fahari Sana kujitambulisha kuwa yeye ni mwanajamaat maduka yake yalisheheni vitabu vya jumuia ambavyo aliviuza kwa kuvieleza maudhui yaliyomo. Mizigo yote ya jamaat alipokua Iringa kituo chake cha kufikia palikua MY STUDIO, duka lake maarufu mjini Iringa. Shughuli zote za pale Iringa zinazohusu jamaat hakukosa. Hata na malezi pale nyumbani kwake yalienda vizuri kwani binti yake anaonyesha mapenzi makubwa ya Jamaat na tayari anao mswada wa kitabu kinachohusu ***Taasisi ya ukhalifa katika Ahmadiyy***a.
Tunashauriwa siku zote kua vipaji tulivyopewa na Allah tuvitumie vizuri ili kuendeleza ujumbe wa Masihi aliyeahidiwa Hadhrar Mirza Ghulam Ahmad(as).

Wanajamaat wameitikia wito huu,Sh Abdul Rahman Ame, Mw Abdallah Mbanga, Mw Khamis Wamwera wametumia vizuri kipaji chao Cha ushairi katika kueneza ujumbe wa Ahmadiyya.Muhammad Rafique alikua mtunzi mzuri wa mashairina lugha yake ya kiswahili ilikua fasaha Sana.

Mara kwa Mara alitunga mashairi kwa ajili ya vikao vya jamaat na alikua na sifa nyingine ya zaidi ambayo washairi wengi hawana ,ustadi wa kughani. Kipaji hiki alikitumia vizuri katika kufikisha ujumbe wa Masihi aliyeahidiwa.

Waaminio ni wale wanaohurumiana wao kwa wao.Muhammad Rafique alikua na mapenzi makubwa na wanajamaat .Hakukubali kuona wanajamaat wakihangaika Kama aliweza kusaidia.

Wanajamaat Alhamdulillah wamepata taaluma ya kupiga picha na vitu vyenye mnasaba na taaluma hiyo Utamaduni huu wa kusaidiana ni muhimu kwa maendeleo ya wanajamaat .Historia Ina mifano mingi ya wanajamaat waliowasaidia wanajamaat wenzao na wakaendelea.Hili ni somo kubwa alilotuachia Muhammad Rafique na litakua Jambo la maana tukifata mfano huu.

MATUKIO KATIKA PICHA

JAMIA AHMADIYYA WAFANYA WAQAR-E-AMAR KATIKA SHULE YA MSINGI JUHUDI.

Mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali hapa nchini zimeendelea kuleta madhara ya aina mbalimbali ikiwemo maafa pia .Halmashauri ya manispaa ya Morogoro ni miongoni mwa sehemu zilizo athirika zaidi na mvua hizo.



Baadhi ya barabara zimeharibika vibaya, baadhi ya nyumba za makazi zimeanguka na nyingine kuzingirwa na maji na baadhi ya majengo ya taasisi za uma kuingiliwa na maji na kujaa tope.

Kufuatia hali hiyo, Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib Mkuu wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya na Naib Amir hapa nchini , aliitisha kikao cha dharura [cha Staff wa Jamia] mara baada ya sala ya Ijumaa ya Tarehe 26/01/2024 ilikujadili nini kifanyike katika kipindi hiki.Baada ya mashauriano ,ilikubaliwa kuwa ufanyike utafiti ni sehemu gani yenye uhitaji zaidi. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa shule ya msingi 'JUHUDI' ya serikali iliyopo katika kata ya Lukobe ndiyo iliyo athiriwa zaidi na mafuriko. Hivyo ikaamuriwa kuwa mpango wa Waqar-e-amar uelekezwe hapo .Baada ya kukamilisha taratibu zote, asubuhi na mapema siku ya Ijumamosi ya tarehe 27/01/2024 kikosi kazi cha vijan wapatao 25 wakiongozwa na Maulana Sheikh Azizi Ahmad Shahzad Sahib kwa maelekezo ya Principal sahib akisaidiana na



Mwl.Kasimu A. Mgalu sahib na Mwl.Abdallah R. Rundo sahib kikaelekea huko kwa jazba na shauku kubwa ya kufanya kazi hiyo muhimu na yenye heshima, kazi iliyofanyika ni kutoa maji na kuzoa tope na kudeki madarasa ,vyoo nk.

Viongozi mbalimbali walikuwepo kama vile Mwenyekiti wa mtaa ,Mwalimu mkuu wa shule hiyo ,Mratibu wa elimu wa kata hiyo pamoja na diwani , wote walitoa pongezi na
shukrani nyingi kwa ujasili wa kujitolea ulioonyeshwa na vijana wetu .

MKUU WA CHUO ASHIRIKI KATIKA ZIARA YA MSTAHIKI MEYA.

Wakati mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya Sheikh Abid Mahmood Bhatti sahib akielekea katika shughuli hiyo ya Waqar-e-amar akipewa taarifa ya kuwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Morogoro anfanya ziara katika kata ya mazimbu ilikukagua na kujionea uharibifu uliosababishwa na mafuriko ,akaona ni vyema nae aungane nae katika ziara hiyo.Ukaguzi huo ulifanyika nyumba kwa nyumba katika maeneo yote yaliyo athirika kwa mafuriko.

Hakika ilikuwa kazi ngumu mno kutembea katika maji yaliyofikia kina cha futi mbili hadi tatu



NABII NI SIMBA WA ALLAH

Na.
Maulana Sheikh Shahab Ahmad

Mwenyezi Mungu Anapomtuma nabii duniani humwondolea hofu moyoni mwake kiasi hiki kwamba hana hofu kabisa ya mtu yeyote isipokuwa ya Allah pekee. Nabii huyo ni simba wa Allah na huwa anakabiliana na changamoto zote kwa uthabiti wa moyo na uimara wa roho. Vikwazo na changamoto hata zikiwa nyingi haziwezi kumwondoa nabii mbali na kazi ya kuhubiri dini ya Mwenyezi Mungu. Hivyo nabii huyo katika zama zake anakuwa ni mfano wa ujasiri mkubwa watu wengine.

Kama manabii wengine Masihi aliyeyahidiwa (as) aliwahi kupata shida na changamoto nyingi maishani mwake naye alikabiliana nazo kwa uthabiti. Wapinzani wake walionyesha nia mbaya na kutumia maneno machafu dhidi yake; na zaidi ya hayo walifungua kesi nyingi dhidi yake ili wajitahidi kumuua kabisa. Lakini simba huyo wa Allah hakukaa nyuma bali alivumilia mateso yote na akawajibu wapinzani kwamba mimi ninamtawakali Allah tu. Hakuna anayeweza kushinda dhidi yangu. Aliwatangazia watu wengi sana kwamba mimi nimelindwa na ulinzi maalumu na msaada makhsusi wa Mwenyezi Mungu kwani yeye ndiye Alinitwisha mzigo wa kiroho naye daima Ataendelea kunisaidia.

Hapo chini ningependa kunukuu baadhi ya maandiko yake kama mfano wa kuonyesha jinsi Masihi Aliyeahidiwa (as) alivyoamini kwamba hawezi kushindwa dhidhi ya wapinzani. Aliwaita wapinzani wathubutu kumpinga simba wa Allah lakini hakuna aliyefanikiwa kujitokeza. Allah alimpa jina la JARIYULLAHI yaani askari hodari wa Allah.

HAMWEZI KUNIUA

"Sifahamu nimewakosea nini, kawaida yangu ni kueleza ukweli ustaarabu na upole, lakini kwa sababu watu hawapendi kuacha uongo kwa namna yoyote ile na kwa mujibu wangu dhambi kubwa kabisa ni kutokusema neno la ukweli na kutokufikisha kwa watu elimu safi iliyong'aa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mji wa maana siogopi vitisho vyao vya kuniua kwani hawawezi kuniua bila mpango wa Mungu. "

(Shahna-e-Haq, Ruhani Khazain, Juz. 2, UK. 326)

SIWAOGOPI WATU

"Enyi Waariya, msinitishe kwa mauaji. siogopi katu vitisho dhaifu vya namna hii, nitang'olea mbali uongo na kufichulia uhakika wa vitabu vyenu vya Veda."

(Shahn-e-Haq, Ruhani Khazain, Juz. 2, UK. 330)

KUNA YEYOTE ANAYETAKA KUJITOKEZA KUKABILIANA NAMI?

"basi hao mabwana waliotajwa hapo juu wajitokeze mbele yangu. Na kama hao wote wakisita, basi Maulawii Rashid Ahmad Gangohi apige moyo konde kujitokeza, maana yeye ndiye mwanakundi wa kwanza wa kundi la Masuni. Pamoja naye yeyote anaweza kushiriki ambaye ni miongoni mwa masufii, vizazi wa masufii na warithi wa masufii maarufu, na sawa na hawa Masheikh ananichukulia mimi kuwa kafiri, mzushi, mwongo na mjanja. Na kama hao wote wahepe kushindana na kwa kutoa udhuru mbovu usioingia akilini wasite kabisa kuukubali mwito wangu huu, basi hoja ya Mungu imekwishatimia juu yao. Mimi nimetumwa na nimepewa bishara ya ushindi. Hivyo, ninawaita mabwana waliotajwa juu kwenye mashindano. Je yuko yeyote atakayekuja mbele yangu?"

(Amani Fesla, Uamuzi wa Kimbingu, Ruhani Khazain, Juz. 4, UK. 325)

MWENYEZI MUNGU HATONIPOTEZA KATU

"Ninakiri kwa kula kiapo cha Mwenyezi Mungu kuwa kama mimi nikishindwa katika mashindano haya, mimi mwenyewe nitachapisha ikirari ya upotofu wangu. Hapo Sheikh apeperushi vya Nadhir Husain na sheikh Batalawii hawatakuwa na haja ya kunikufurisha. Na katika hali hii mimi ndiye nitastahili kila dhila, shutuma na fedheha na nitakiri katika mkutano huo huo kuwa mimi sikutoka kwa Mwenyezi Mungu na madai yangu yote ni batili. Na Wallahi nina yakini na ninaona kuwa Mungu wangu kamwe Hatafanya hivyo na Hataniacha nipotee bure."

(Amani Fesla, Uamuzi wa Kimbingu, Ruhani Khazain, Juz. 4, UK. 330)

HAWAWEZI KUZIMA NURU YA ALLAH

"Alama kubwa sana watu hawa wanafanya juu chini kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu na wanatumia kila namna ili kuwapotosha watu na wanatumia nguvu zao zote, wanatoa fatwa za kukufurisha, na wanasuka njama za kuniudhi. sheikh batalwi amewahimiza watu waende kuilalamikia serikaliini dhidi yangu, ilmuradi hawajaacha hila yoyote na wamewakusanya watu wengine pia katika uongo wao. niliwahi kumuarifu sheikh batalwi le kwa kupata ufunuo wa Mwenyezi Mungu lakini Mwenyezi Mungu yu pamoja nami. kwa sasa hali ile ile inatokea na watu wameamua kufanya waadui kwamba hata familia wameacha uhusiano. pamoja na haya yote hatimaye mimi nitashinda, nayo itakuwa alama kubwa ya ukweli wangu. na hizi zote ni alama za ukweli wangu ambazo ni neema nilizopata kwa Mwenyezi Mungu. angaliaeni Mwenyezi Mungu anasema ndani ya quran tukufu ni mdhalimu mkubwa nami ninamkamata muongo upesi na simpi muda. lakini kwa sasa huu ni mwaka wa 11 unaendelea tangu nitangaze kuwa Mujadidi na mfano wa masihi na mwenye kupokea ufunuo wa Mwenyezi Mungu. je hii si alama ya ukweli? kama kazi hii isingelikuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu inawezekanaje kustawi kwa miaka 10 ambayo ni sehemu kubwa ya umri wa mtu. tena narudia kusema je hii si alama ya ukweli kwamba yeyote anayeweza kukabiliana na mimi mnyenyekevu kwenye utabiri na akijitokeza fedha na vivyo hivyo mamia ya alama za msaada wa Allah zinaonekana. mimi ni bustani ya Mwenyezi Mungu atakayeamua kunikata atakatwa mwenyewe, adui atafedheheka na atakayekataa atajuta. hizi zote ni alama za kweli kwa apendaye kuona."

(Nishan-e-Asmani, Ruhani Khazain, Juz. 4, UK. 397-398)

MIMI SIWEZI KUKOMA KWA SABABU YA WATU

"Mimi ninamshukuru Mwenyezi Mungu mkarimu kwa sababu hii pia kwamba alinijalia moyo wa kusambaza dini ya uislamu. kwa fadhila ya mwezi Mungu sioni aibu ya kujitolea maisha kwa ajili ya kazi hii kubwa. mimi nimeshaacha tamaa na watu wa dunia lakini kikubwa ninamtegemea Mwenyezi Mungu. mimi ninaelewa kwamba hata kama mimi niko pekee yangu lakini kwa hakika siko pekee yangu mola wangu yu pamoja nami mwingine karibu na mimi kuliko yeye. kwafadhila yake yeye nilipata roho hii ya upendo kwamba niendelee kuitumikia dini licha ya mateso mnanifanya kazi za kiislamu kwa shauku na moyo mkunjufu."

(Aina Kamalat e Islam, Ruhani Khazain, Juz. 5, UK. 35)

JUMUIYA YANGU HAIWEZI KUANGAMIA

"Watu hawa hawapendi isipokuwa wazime nuru ya mwenyezi mungu kwa vinywa vyao lakini haiwezi kuzimika kwa sababu Mwenyezi Mungu aliwasha mwenyewe. sijui kwa nini wanajitaabisha kwa kunikadhibisha. kama hapa duniani kuna yeyote ambaye amesaidiwa kama mimi naitwa na anakadhibisha madai yangu ya kuwa Masihi Aliyeahidiwa[as] basi kwa nini hajitokezi kushindana nami? wanaendelea na kawaida kama wanawake. daima makafiri wasio na staha huwa wanafanya hivi lakini kama nimesimama nikiwa na watu wenye akili, Maulamaa na watawa wapatao elfu 30 na alama nyingi za mbinguni zinaendelea kudhihirika sasa je jumuiya hii Mwenyezi Mungu inaweza kuangamia? la hasha. haiwezi kuangamia. bali wataangamia wale tu wanaopenda kuuangamiza mpango wa Mungu."

(Tohfa Golarwiya, Ruhani Khazain, Juz. 17, UK. 180-181)

YUKO NAMI KATIKA KILA HATUA

"Ninaapia kwa Mwenyezi Mungu mkarimu mwenye nguvu ni adui wa uongo naye ni mwenye kumwangamiza mzushi kwamba mimi nimetokana na Yeye na mimi naitwa kwa wakati muafaka kwa sababu yeye aliniituma na nimesimama na amri yake naye yuko nami kwa kila hatua. yeye hawezi kunipoteza wala hataipoteza jumuia yangu mpaka pale atimize malengo yake aliyoyakusudia."

(Arba'iin, Ruhani Khazain, Juz. 17, UK. 348)

Maisha ya Masihi Aliyeahidiwa (as) yamejaa matukio ambapo alisaidiwa na Mwenyezi Mungu hata kama kidhahiri mazingira hayakuwa rafiki. Ni jukumu letu kusoma zaidi kuhusu maisha yake ili kupata elimu juu ya msaada wa Allah uliopatikana katika hatua zote. Allah Atujaalie sana. Aamin

Mtume Mtukufu[saw] – Mfano Mkuu

Matukio katika Maisha ya Mtukufu Mtume[saw]

Kutoka uk. 12

yafikishwe kwa Mtukufu Mtume (saw). Aliomba afahamishwe Mtukufu Mtume (saw) kwamba alikuwa amevumilia majeraha 12 ya mkuki, lakini kwamba mtu yeyote ambaye alikuwa amekutana naye ana kwa ana katika vita aliuawa. Alisema kwamba watu wake wanapaswa kuambiwa kwamba kama Mtukufu Mtume (saw) atauawa kishahidi wakiwa wao bado hai, basi hakutakuwa na udhuru kwao. Kwa maneno mengine, wanapaswa kutoa maisha yao ili kumlinda Mtukufu Mtume (saw) na Uislamu. Haya ndiyo yalikuwa mapenzi ya Maswahaba hata katika pumzi zao za kufa. Baada ya haya, Hadhrat Sa'd (ra) alifariki na akawa shahidi. Mtukufu Mtume (saw) aliposikia habari hizi, aliomba rehema kwa Hadhrat Sa'd (ra) na akasema kwamba yeye ni mwenye mapenzi mema kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (saw) katika maisha yake na kifo chake.

Matendo ya Kishenzi katika Vita vya Makafiri

Khalifa Mtukufu (atba) amemnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye anaandika:

Sasa Mtukufu Mtume (saw) pia alikuwa ameshuka kwenye uwanja wa vita na kazi ya kutunza miili ya mashahidi ilikuwa ikiendelea. Wakati huo, maono yaliyokuwa mbele ya Waislamu yalikuwa ni kutoa machozi ya damu. Waislamu sabini walikuwa wametanda katika uwanja wa vita wakiwa wametapakaa kwa vumbi na damu, na walionyesha mandhari ya kuogofya ya mapokeo ya kishenzi ya Kiarabu yanayojulikana kama Muthlah. Miongoni mwa waliopoteza maisha, kulikuwa na Muhajrina sita tu na wengine wote walikuwa kutoka kwa Ansari. Idadi ya watu waliouawa miongoni mwa Maquraishi ilikuwa ishirini na watatu. Mtukufu Mtume (saw) alipokuja kwenye mwili wa ami yake na kaka yake wa kambo, Hamzah bin Abdil-Muttalib (ra), alipigwa na butwaa kwa sababu Hind, mke mshenzi wa Abu Sufyan alikuwa ameharibu vibaya sana maiti yake. Kwa muda fulani, Mtukufu Mtume (saw) alisimama pale kimya kimya, na dalili za huzuni na hasira zilidhihirika kwenye uso wake. Kwa muda kidogo, Mtukufu Mtume (saw) alijiwazia mwenyewe kwamba mpaka wanyama hawa wa Makka wenye kiu ya damu wasipoonja ladha ya dawa yao wenyewe (nao miili ya maiti zao ikatwe katwe), labda hawatapata fahamu zao, lakini Mtukufu Mtume (saw) akajizuia kutoka kwenye wazo hili na kuonyesha uvumilivu. Kwa hakika, baada ya hayo, Mtukufu Mtume (saw) alikataza desturi ya Muthlah katika Uislamu milele, na akasema kwamba adui anaweza kufanya apendavyo, lakini Waislamu kwa vyovyote vile wanapaswa kujiepusha na tabia hiyo ya kishenzi, na kufuata njia ya wema na ihsani.

(Maisha na Tabia ya Muhuri wa Manabii (sa) , Juzuu 2 , uk. 344-345)

Khalifa Mtukufu (atba) zaidi amemnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye anaandika:

'Maquraishi walikuwa wameifanyia unyama ule miili ya maswahaba wengine pia. Kwa hiyo, mwili wa Abdullah bin Jahash (ra), binamu wa baba yake Mtukufu Mtume (saw) pia ulikuwa umeharibika vibaya sana. Kadiri Mtukufu Mtume (saw) alivyokuwa akihama kutoka kwenye mwili mmoja hadi mwingine, dalili za uchungu na maumivu zingedhihirika zaidi na zaidi kwenye uso wake.'

(Maisha na Tabia ya Muhuri wa Manabii (sa) , Juzuu 2 , uk. 345)

Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad (ra) ambaye anasisitiza kwamba katika maneno yake ya kufa, Hadhrat Sa'd (ra) hakueleza au kujiuliza ni nani angeitunza familia yake baada ya yeye kuondoka. Badala yake, wasiwasi wake pekee na maneno yake ya mwisho yalikuwa juu ya kumlinda Mtukufu Mtume (saw) na kuhakikisha kwamba Waislamu wangetoa maisha yao kwa kufanya hivyo.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba mtu anastaajabia aina hizi za maonyesho ya upendo kwa Mtukufu Mtume (saw). Khalifa Mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aimarishe roho hii ya upendo kwa Mtukufu Mtume (saw) ndani yetu pia. Tunapoanzisha njia hizo za kufikiri, basi sisi pia tutaongezeka katika uhusiano wetu na Mwenyezi Mungu na tutajitahidi kikweli kuondoa udhaifu wetu ili roho ya kweli ya Kiislamu iimarike katika ibada zetu, mwenendo wetu wa kimaadili na tabia zetu.

Sala ya Jeneza

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba ataongoza sala ya jeneza ya wafu wafuatao:

Dkt Mansoor Shabooti; Dkt Mansoor Shabbooti wa Yemen. Alikuwa mfungwa katika njia ya Allah huko Yemen, na alikuwa amefungwa kwa sababu ya imani yake ya Uahmadiyya. Ilikuwa wakati wake gerezani kwamba aliaga dunia. Kwa namna hii, kwa kuwa alifungwa kwa sababu ya imani yake, anahesabiwa kuwa shahidi. Kwa hivyo, yeye ndiye shahidi wa kwanza wa Ahmadiyya huko Yemen. Ameacha mama yake mzee, mke wake na wanawe wawili. Kwa vile wanaume wengi wa Ahmadiyya huko Yemen wamefungwa, sala yake ya mazishi ilisaliwa huko Yemen na wasiokuwa Ahmadiyya. Baba yake alikuwa Ahmadiyya wa kwanza nchini Yemen. Mwanawe anaeleza jinsi watekelezaji sheria walivyoingia nyumbani kwao, na kuweka bunduki kichwani mwake na kusema kwamba alikuwa anapokea pesa kutoka nje ya nchi. Mansoor Shabbooti alikanusha hilo, akisema chochote alichonacho ni matokeo ya bidii yake, hakuna kutoka nje ya nchi. Khalifa Mtukufu (atba) alitoa maoni yake kwamba haya ni masingizio ya kawaida ambayo wale wanaojiita masheikh wanajaribu kuyatoa dhidi ya Waahmadiyya, wakisema kwamba tunachukua pesa kutoka kwa madola ya Magharibi na tuna aina fulani ya ajenda dhidi ya Uislamu. Ingawa ukweli ni kwamba kila Ahmadiyya anajitolea fedha kwa ajili ya kueneza ujumbe wa Uislamu kwa ulimwengu na kuwatumikia wanadamu. Mke wa Mansoor Shabbooti alisema baadaye alionyeshwa chumba alichokuwa amefungwa, na walinzi walimwambia kwamba mara nyingi wangesikika akilia katika maombi. Pia walimthibitishia kwamba alikuwa amefungwa kwa sababu ya taarifa kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya ilimtumia pesa kutoka nje ya nchi ambazo alizitoa kwa majeshi ya Malaysia. Hizi ni aina za tuhuma za uwongo wanazotunga. Walisema baada ya uchunguzi walibaini kuwa madai hayo si ya kweli na walikuwa karibu kumwachilia huru.

Ndugu yake anaandika kwamba alikuwa mkarimu sana. Alikuwa na elimu nzuri sana, mara kwa mara katika kuswali, kusoma Qur-aan na kutoa sadaka. Angewatendea maskini na wahitaji bure na angepoteza ada zake mwenyewe. Alikuwa na shauku ya kueneza ujumbe wa Uislamu na hata angeweza kuwahubiria maprofesa wake wa chuo ambao wangesikiliza kile alichosema.

Alimaliza PhD yake huko Jordan, ambapo alikuwa akisafiri saa moja kila Ijumaa ili kuhudhuria sala ya Ijumaa. Angedumisha uhusiano mzuri na jamaa zake wote, wakiwemo wale ambao hawakuwa Ahmadiyya. Alipendwa na Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya vile vile. Muungano wa madaktari nchini Yemen pia ulitoa taarifa ya rambirambi na kueleza uzito mkubwa wa hasara yake. Alitumia maisha yake kuwatumikia wanadamu, na Mungu alikuwa ameweka uponyaji mkononi mwake. Ahmadiyyat imeenea Yemen kwa kiasi kikubwa kwa sababu yake. Khalifa Mtukufu (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu amtendee marehemu kwa msamaha na rehema, anyanyue daraja yake, na awape subira na nguvu familia yake. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) pia aliomba kwa ajili ya kuachiliwa kwa haraka kwa wale Waahmadiyya waliokuwa bado wamefungwa huko Yemen.

Salahuddin Muhammad Saleh Abdul Qadir Odeh; Salahuddin Muhammad Saleh Abdul Qadir Odeh ambaye alikuwa babake Sharif Odeh, Rais wa Kitaifa wa Jumuiya ya Kababir. Ameacha mke na wanawe watatu, Muhammad Sharif Odeh, Munir Odeh na Amir Odeh pamoja na binti, Manal Odeh. Wajukuu zake wawili wanasoma katika Jamia Ahmadiyya. Alizaliwa Ahmadiyya kama ambavyo baba yake, babu na babu wa baba yake wote walikuwa Ahmadiyya.

Alipokuwa mdogo, alipoteza fahamu kutokana na baridi kali. Baada ya kufikishwa hospitalini, madaktari walitoa maelezo mabaya sana, wakisema kwamba nafasi yake ya kuishi ilikuwa ndogo sana na kwamba hata kama angepona hataweza kupata watoto. Barua ilitumwa kwa Khalifa wa Pili (ra) kwa ajili ya maombi, na akaendelea kuishi, kuoa na kupata watoto. Alikuwa mstari wa mbele katika kuitumikia Jumuiya na alikuwa na shauku kubwa ya kuwahudumia wageni wa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Ukarimu wake ulijulikana sana hivi kwamba watu wangetaka kukaa naye ili tu waone ukarimu wake. Pia aliwatunza maskini na wahitaji.

Mwendelezo wa Hotuba hii unapatikana katika vituo vyote, kwa njia ya mtandao na Karatasi.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 10

Nabii ni Simba wa Allah



HABARI UK> 8

TANGAZO

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah Tanzania

Mtume Mtukufu^{saw} – Mfano Mkuu

Matukio katika Maisha ya Mtukufu Mtume^{saw}

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatihah, Khalifa Mtukufu Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisema kwamba amekuwa akitaja kauli mbiu za masanamu zilizotolewa na Abu Sufyan katika tukio la Vita vya Uhud, na za Mtukufu Mtume (saw) mwitikio na maagizo ya kuinua kauli mbiu za utukufu wa Mungu.

Majibu ya Maneno ya Abu Sufyan Wakati wa Vita vya Uhud

Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad (ra) ambaye alieleza kwa kina jinsi Abu Sufyan alivyoyatukuza masanamu yake alipofikiri kwamba Mtukufu Mtume (saw) ameuawa. Kwa kujibu, Mtukufu Mtume (saw) aliwaagiza masahaba wake kutangaza ukuu wa Mwenyezi Mungu, na kusema kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa Mlinzi wao ambapo makafiri hawakuwa na mlinzi.

Khalifa Mtukufu (atba) alizidi kumnukuu Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad^{ra} ambaye anaandika kwamba wakati Abu Sufyan alipokuwa akitangaza habari za uongo kwamba Mtukufu Mtume^{saw} ameuawa, Mtukufu Mtume^{saw} aliwaagiza masahaba wake kunyamaza. Aliamuru vivyo hivyo wakati habari za uwongo za mauaji ya Hadhrat Abu Bakr (ra) na Hadhrat Umar (ra) zilipokuwa zikitangazwa. Lakini Abu Sufyan alipoanza kuyatukuza masanamu yake, Mtukufu Mtume (saw) hakuweza kunyamaza kwani utukufu wa Mungu ulikuwa ukitiliwa shaka. Na kwa hivyo, licha ya kukaa kimya hapo awali, sasa Mtukufu Mtume (saw) aliwaagiza masahaba kutangaza kwamba utukufu wa kweli ni wa Mungu peke yake.



Muhtasari wa hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} ilitolewa Tarehe 21 Mwezi wa Februari, 2024

Mauaji ya Hadhrat Hanzalah (ra) na Hadhrat Sa'd bin Rabi' (ra)

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alitoa maelezo kuhusu kuuawa kishahidi kwa Hadhrat Hanzalah (ra) na Hadhrat Sa'd bin Rabi' (ra). Hadhrat Hanzalah (ra) aliuawa kishahidi katika Vita vya Uhud baada ya kuowa siku moja tu kabla ya vita kuanza. Mtukufu Mtume (saw) aliwaona malaika wakiosha mwili wake kwenye uwanja wa vita. Hadhrat Sa'd bin Rabi' (ra) pia aliuawa kishahidi katika Vita vya Uhud. Mtukufu Mtume (saw) aliomba mtu aende na kujua kuhusu Sa'd (ra) kutoka kwenye uwanja wa vita. Sahaba mmoja alikwenda kumtafuta na alipompata Sa'd (ra), sahaba huyo akamwambia kwamba Mtukufu Mtume (saw) alikuwa anauliza kuhusu yeye. Hadhrat Sa'd (ra) aliomba maamkizi yake ya 'Salam'

UK. 11



Je, Wajua?

Je wajua kuwa moto huwaka kwa sababu ya muunganiko wa vitu vitatu. Joto, hewa ya oksijeni na fuel (kitu chochote kinachoweza kuwaka, mfano mbao, mafuta n.k). kikitolewa kitu kimojawapo katika hivyo wakati moto unawaka, basi moto utazima. Hivyo zimamoto huwa wanajaribu njia zote ili waondoe kitu kimojawapo kati ya hivyo vitatu ili moto uzimike. Maji yanatumika kutoa hali ya ujoto, japo joto likiwa kali sana basi maji hayawezi kupunguza joto kiasi cha kuzima moto.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com